

## MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

### 1. Kwa nini utumie Mfumo huru wa kupokea malalamiko?

IRM inasaidia mradi ulioathiri watu au jumuia kutatua na kushughulikia shida kwa njia ya mazungumzo au kufanya uchunguzi kwa njia ilio huru, haki na inayozingatia muda.

### 2. Je! Kufungua malalamiko husimamisha mradi?

Hapana. Uamuzi wa kusimamisha mradi upo chini ya maamuzi ya Sekretarietii au Bodi ya GCF kuzingatia matokeo ya mchakato wa IRM.

### 3. Je! Kuna vikwazo vyovyothe vya muda wa kufanya malalamiko?

Ndio. Malalamiko lazima yapelekwe ndani ya miaka miwili (2) ya tarehe ambayo mlalamikaji alitambua athari mbaya za mradi wa GCF, au ndani ya miaka miwili (2) baada ya kufungwa kwa mradi wa GCF.

### 4. Je! Nitarajie matokeo gani baada ya kufungua malalamiko na IRM?

Kumpatia mlalamikaji jibu kwa wakati, kuwa na mchakato huru na wa haki katika kushughulikia maswala yanayohusiana na mradi moja kwa moja au kupitia uchunguzi huru ambao unaweza kupendekeza marekebisho. Matokeo maalum hutegemea adhari zilizoainishwa katika malalamiko.

### 5. Je! IRM hutofautiana vipi na utaratibu wa kupokea malalamiko kwa ngazi ya mradi?

IRM ni njia nyingine ambayo mradi ulioathiri watu unaweza kufanyiwa marekebisho, haswa kwa wakati ambao taratibu na sheria za GCF hazikufuatwa vyema. IRM inahimiza utumiajui wa mifumo ya malalamiko iliyowekwa na mamlaka husika katika ngazi za mitaa

## WASILIANA NASI

### INDEPENDENT REDRESS MECHANISM

#### Green Climate Fund

Songdo Business District  
175 Art Center-daero  
Yeonsu-gu, Incheon 22004  
Republic of Korea

✉️ [irm@gcfund.org](mailto:irm@gcfund.org)

📞 +82.32.458.6485

🏡 <https://irm.greenclimate.fund/>

🐦 @GCF\_IRM



## GCF INDEPENDENT REDRESS MECHANISM

KUFUNGUA MILANGO  
YA UWAJIBIKAJI NA  
KUREKEBISHA

## KUHUSU SISI

---

**Mfumo huru wa kupokea malalamiko ni mfumo wa uwajibikaji na utaratibu wa kurekebisha hali ya hewa, mfuko wa ulimwengu ulioundwa kusaidia nchi zinazoendelea kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa kwa kupunguza uzalishaji wa gesi chafu na kupambana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa. IRM iko huru na inajitegemea yenyewe na inaripoti moja kwa moja kwenye Bodi ya GCF.**

## JUKUMU LETU

---

Dhamira kuu ya IRM ni kushughulikia malalamiko ya watu ambao wanaamini wameathiriwa vibaya na miradi ya GCF, pia kuisaidia GCF kuwa mwaminifu na kuwajibika kulingana na sera na taratibu ilizojiwekea.

## JINSI YA KUFANYA MALALAMIKO

---

**Ni malalamiko gani yanayoweza kushughulikiwa na IRM?**

Mtu yeyote, kikundi au jumuia inayoamini kuwa wamedhuriwa, au wanaweza kudhuriwa na mradi wa GCF pamoja na wale wanaotegemea madhara wanaweza kuwasilisha malalamiko.

**Habari gani zinahitajika?**

Hakuna fomu maalum inahitajika kupeleka malalamiko. Ijapokuwa, malalamiko yanapaswa kujumuisha habari ifuatayo:

- Jina na taarifa za mawasiliano ya mtu au jumuia ya watu wanaowasilisha malalamiko
- Maeleo mafupi ya mradi au mpango uliofadhliliwa na GCF
- Maeleo ya madhara au athari zilizosababishwa na mradi
- Ikiwa imewasilishwa na mwakilishi, barua kutoka kwa watu walioathirika au jumuia iliyomruhusu mwakilishi kuwasilisha malalamiko kwa IRM

IRM inakubali malalamiko katika lugha yoyote. Wanaweza kuwasilishwa kwa njia ya barua, barua pepe, faksi, au kuwasilisha binafsi kwa anwani iliyo nyuma ya brosha hii. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa kwa maandishi, au kama video au sauti ya kurekodi.

## JE, MALALAMIKO YANASHUGHULIKIWA VIPI?

---

- **Hatua ya kwanza**, IRM huangalia kama malalamiko **yamekidhi vigezo**.
- Kama yamekidhi vigezo, IRM inawezesha **mchakato wa kutatua** na kusuluhiha tatizo **kwa njia ya hiari** na kukubaliana juu ya suluhisho
- Ambapo utatuzi wa tatizo haukuafikiwa au haifanyi kazi, IRM hufanya **tathmini ya malalamiko na kufanya uchunguzi** ili kubaini ukiukwaji wa sharia na masharti ya GCF na kupendekeza kurekebisha
- IRM inasimamia na **kufuutilia** utekelezaji wa makubaliano ya utatuzi wa malalamiko yoyote yaliyoafikiwa na bodi ya GCF au marekebisho yoyote ambayo yamefanywa na bodi ya GCF

*IRM inaheshimu maombi ya usiri kutoka kwa walalamikaji na itaweka habari ilizopokea kwa washirika wake kwa siri kutoka kwa watu wengine mbali na IRM, isipokuwa kama kuna makubaliano yaliyokubaliwa vinginevyo. IRM haikubali malalamiko bila majina.*